# BUNGE LA TANZANIA

---

## BUNGE LA KUMI NA MBILI

---

## MKUTANO WA KWANZA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### Kikao cha Kwanza – Tarehe 10 Novemba, 2020

*(Mkutano Ulianza Saa 3:05 Asubuhi)*

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**TANGAZO LA RAIS LA KUITISHA MKUTANO WA BUNGE**

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

Naomba tukae tuanze, walioko nje waingie tuanze kazi, tutasalimiana baada ya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane tafadhali, kama ambavyo *Order Paper* yetu inaonesha naomba niwasomee Tangazo la Mheshimiwa Rais la Kuitisha Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa masharti ya Katiba, Mkutano huu wa Kwanza wa Bunge jipya unaanza kwa Mheshimiwa Rais kuitisha, hivyo naomba kuchukua nafasi hii kusoma Tangazo la Mheshimiwa Rais kama ambavyo nimelipokea.

Tangazo la Serikali Namba 942(a) la tarehe 5 Novemba, 2020. Hati ya kuitisha Mkutano wa Bunge jipya iliyotolewa kwa mujibu wa Ibara ya 90(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

KWA KUWA, Uchaguzi Mkuu ulifanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977;

NA KWA KUWA, masharti ya Ibara ya 90(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inamtaka Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kuitisha Mkutano wa Bunge jipya kabla ya kupita siku saba tangu Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutangaza matokeo ya Uchaguzi Mkuu;

NA KWA KUWA, matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 yalitangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi tarehe 30 Oktoba 2020;

HIVYO BASI, mimi John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mamlaka niliyonayo chini ya Ibara ya 90(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ninaitisha Mkutano wa Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ufanyike katika Ukumbi wa Bunge uliopo Mjini Dodoma tarehe 10 Novemba, 2020 kuanzia saa 03:00 asubuhi.

Kwa kuthibitisha ninaweka saini yangu na muhuri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hati hii leo tarehe 5 Novemba, 2020.

Mwisho wa kunukuu na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa hivi tutakwenda kwa utaratibu wa kumpata Mwenyekiti wa muda kwa sababu baada ya hapa tutakuwa na uchaguzi wa Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 9(4) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 inaweka masharti ya Uchaguzi wa Spika kufanyika katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge jipya mara ya baada ya Katibu kusoma Tangazo la Mheshimiwa Rais na kikao hicho kujigeuza kuwa

Mkutano wa Uchaguzi wa Spika. Aidha, Kanuni ya 9(5) inaweka masharti ya Uchaguzi wa Spika kusimamiwa na Mwenyekiti ambaye atatoka miongoni mwa Wabunge ambao wamekuwa Wabunge mfululizo kwa muda mrefu na asiye mgombea wa nafasi ya Spika baada ya kuombwa na Katibu kuongozo Kikao cha Uchaguzi wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge ambaye anakidhi vigezo vilivyoainishwa na Kanuni ya 9(5) ni Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ambaye Bunge hili la Kumi na Mbili ndiye Mbunge wa muda mrefu aliyedumu tangu mwaka 1995. *(Makofi)*

Hivyo namuomba Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ajongee mbele kukalia kiti hiki na kuwa Mwenyekiti wa Uchaguzi huu wa Spika. *(Makofi)*

*Hapa (Mhe. William V. Lukuvi) Alikalia Kiti*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, karibuni sana katika ukumbi huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliopo hapa Makao Makuu, Dodoma. Namshukuru Mungu sana kwa niaba yenu kwa kutuwezesha wote kushiriki uchaguzi salama na kuchaguliwa na kuaminiwa na wananchi kuingia kwenye ukumbi huu. Lakini pia tunamshukuru Mwenyezi Mungu kukamilisha zoezi zima la uchaguzi ambalo tumempata Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Rais wetu katika kipindi cha pili na sisi kama wawakilishi wa wananchi wa Bunge hili kuchaguliwa.

Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu ya leo kama mlivyomsikia kutoka kwa Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ni Katibu wa Bunge ni kumchagua Spika. Lakini kabla hatujaanza kazi hiyo nadhani ni wajibu wangu kama nilivyoanza mwanzo kuwapongeza sana kwa ushindi mlioupata na kuaminiwa na wananchi kuja hapa Dodoma kuwawakilisha. *(Makofi)*

Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, chama changu, lakini nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wa vyama vingine vilivyoshiriki na wananchi kuwaamini kuja katika jengo hili. Mungu ametupenda sana Tanzania, tumefanya uchaguzi wa amani, uchaguzi ambao umeendeshwa kwa amani, lakini pia kwa haki, uchaguzi ambao umeendeshwa vizuri kwa haki na ambao umetuwezesha sisi kuingia humu Bungeni, kwa hiyo nawapongezeni sana na karibuni sana ndani ya ukumbi huu ili tushiriki katika zoezi hili la awali kabisa.

Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kanuni kutamka kwamba nije kukalia kiti hiki leo, lakini mngeweza mkasimama, mkakataaa na pengine Kanuni ingeweza kubadilishwa, kwa hiyo, nawashukuru sana kwa imani yenu ya kuniamini ambayo mmeonesha kwangu baada ya mimi kuombwa na Katibu wa Bunge kuwa Mwenyekiti wa mkutano huu ambao kazi yake kubwa ni kumchagua Mheshimiwa Spika wa Bunge letu hili la Jamhuri wa Muungano.

Narudia tena kuwapongeza, lakini nampongeza zaidi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kusimamia amani katika kipindi chote cha uchaguzi wetu, lakini na yeye kwa kuchaguliwa katika shughuli zetu za Bunge kama mnavyosoma Katiba, Rais ni sehemu ya Bunge, mambo yetu yote hayakamiliki mpaka sahihi ya Mheshimiwa Rais, kwa hiyo ninayo wajibu kwa niaba yenu kumpongeza na yeye kwa ushindi mkubwa ambao wa kihistoria ambao wameupata katika uchaguzi huu. *(Makofi)*

Baada ya maelezo yangu haya ya utangulizi naomba sasa nijielekeze moja kwa moja kwenye shughuli iliyoko mbele yetu ya kumchagua Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikisomwa pamoja na Ibara ya 68 ya Katiba na kama mlivyoona kwenye orodha ya shughuli za Bunge na ratiba

yetu leo tutakuwa na Uchaguzi wa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shughuli hii ni muhimu sana kwetu, lakini ni muhimu sana kwa Taifa, ni muhimu sana kwa muhimili huu wa Bunge, kwani sisi kama Wabunge hatutaweza kushiriki katika shughuli za Bunge kabla ya kuapishwa Kiapo cha Uaminifu, isipokuwa katika Uchaguzi wa Spika. Kwa maneno mengine tukishampata Mheshimiwa Spika yeye sasa ndio atafanya shughuli ya kutuapisha sisi wengine wote tuliopo humu ndani.

Kwa hiyo, jambo tunalolifanya hili ni muhimu sana kwetu sisi na ningependa Waheshimiwa Wabunge wote tuwe watulivu kwa sababu tunatafuta kiongozi muhimu sana katika nchi hii na katika Bunge letu yaani tunamtafuta Kiongozi wa Bunge letu hili, kwa hiyo lazima tuwe watulivu sana, nawaombeni ili tukamilishe shughuli hii muhimu na tukishamaliza kumpata yeye, yeye ndio atafanya kazi hiyo kuanzia leo ya kutuapisha sisi sote tuliochaguliwa na wananchi kuja kuwawakilisha kwenye Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi ni Katibu wa Bunge naomba sasa nimpe nafasi hii ili atoe maelezo ya utaratibu kuhusu shughuli ya leo hii ya uchaguzi wa Spika. Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Spika wa Bunge anachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni mwa Wabunge au watu wenye sifa za kuwa Wabunge. Aidha, Katiba inaelekeza kwamba uchaguzi wa Spika utafanyika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge jipya na katika Kikao cha Kwanza chochote mara baada ya Kiti cha Spika kuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti ya Katiba niliyoainisha hapo juu, tarehe 5 Novemba, 2020 nilitoa Tangazo Namba 1763(a) katika Gazeti la Serikali Toleo Maalum kuwatangazia kuwa Kiti cha Spika kitakuwa wazi tarehe 10 Novemba, 2020 Bunge litakapokutana kwa mara

ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kwamba Uchaguzi wa Spika utafanyika siku hiyo.

Aidha, niliviarifu vyama hivyo kuwa chama chochote cha siasa chenye usajili wa kudumu kinachokusudia kusimamisha mgombea katika uchaguzi huo kiwasilishe jina la mgombea huyu ofisini kwa Katibu wa Bunge Dodoma kabla ya saa 10.00 jioni ya tarehe 9 Novemba, 2020 ambayo ndio siku ya uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwatangazia pia kuwa chama kinachokusudia kumsimamisha mgombea ambaye sio Mbunge kiwasilishe jina la mgombea huyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili Tume ithibitishe iwapo mgombea huyo ana sifa za kuwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge hili tukufu kuwa hadi kufikia saa 10:00 jioni ya tarehe 9 Novemba mwaka huu nilikuwa nimepokea jina la mgombea mmoja tu ambaye ni Mheshimiwa Job Yustino Ndugai kutoka Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Hata hivyo, ilivyofika saa 12:00 jioni ya tarehe 9 Novemba mwaka huu, ofisi yangu ilipokea barua pepe kutoka kwa Ndugu Boniventura Peter Ndekeja wa Chama cha *National League for Democracy (NLD)* akiomba kuwa mgombea wa nafasi ya Spika. Ndugu Boniventura Peter Ndekeja hajakidhi masharti ya Kanuni kwa sababu zifuatazo:-

Moja, Ndugu Boniventura Peter Ndekeja sio Mbunge, hivyo chama chake kilitakiwa kuwasilisha jina lake Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili Tume ithibitishe iwapo ana sifa za kuwa Mbunge, lakini hakufanya hivyo.

Pili, Tangazo nililotoa kwa mujibu wa Kanuni nilielekeza kuwa jina la mtu anayependekezwa kuwa mgombea wa nafasi ya Spika liwasilishwe Ofisi ya Katibu wa Bunge kabla ya saa 10.00 jioni ya tarehe 9 Novemba, 2020 ambayo ndio ilikuwa siku ya uteuzi, lakini barua pepe ya Ndugu Ndekeja imepokelewa saa 12 jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo Ndugu Boniventura Peter Ndekeja amekosa sifa za kuwa mgombea wa nafasi ya Spika. Hivyo, mgombea aliyekidhi vigezo ni Mheshimiwa Job Yustino Ndugai tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu utakaofuata ni kwamba mgombea huyo atafika mbele yenu kwa kuwa ninyi ndio wapiga kura ili kujieleza kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza kuulizwa na kujibu maswali kama yatakuwepo na kisha kuomba kura.

Baada ya zoezi hilo kukamilika kila Mbunge atapewa karatasi ya kura yenye jina la mgombea na atatakiwa kupiga kura ya ndio au hapana mbele ya jina hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kura zitakuwa za siri ambapo kila Mbunge atapiga kura yake mahali alipoketi na baada ya hapo masanduku ya kura yataletwa hapo mbele yenu yakiwa wazi ili ninyi Waheshimiwa Wabunge kama wapiga kura muweze kuyathibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Mbunge ambaye kabla ya shughuli ya uchaguzi kumalizika atakosea katika kuweka alama kwenye karatasi ya kura ataruhusiwa kumrudishia Katibu karatasi hiyo na papo hapo Katibu ataifuta na kuiharibu na kisha kumpa Mbunge huyo karatasi nyingine ya kura.

Kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, iwapo mgombea huyo atapata kura nyingi za ndio atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Spika wa Bunge.

Baada ya kutoa maelezo hayo ya msimamizi wa uchaguzi ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wamesikiliza vizuri na sasa naomba kukukaribisha ili uongeze zoezi la mgombea kujieleza na kuomba kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Katibu wa Bunge ambaye ndiye msimamizi wa uchaguzi huu.

Waheshimiwa Wabunge, labda kabla sijamuita mgombea kwa faida tu ya Waheshimiwa Wabunge tuliopo humu ndani tupo Wabunge tuliochaguliwa, wapo Wabunge wa Viti Maalum na makundi mbalimbali, lakini labda kwa faida yenu niwatambulishe Mwanashseria Mkuu, Profesa Kilangi. Huyu mwenzetu ni Mwanasheria Mkuu, lakini ni Mbunge, maana msije mkashangaa mkasema tulileta kura mamluki. Lakini kwa heshima hiyo tunaye humu ndani Mbunge wa Ruangwa ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu. *(Makofi)*

Baada ya utambulisho huo mdogo naomba kwa heshima sasa katika hatua hii nimuombe, naomba ruksa yenu nimuite sasa mgombea aliyetajwa ndugu yetu Mheshimiwa Ndugai, Mbunge wa Kongwa ambaye ameteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuja kuwania nafasi hii ya Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ajongee mbee ili tumpe nafasi ya kujieleza. Karibu mbele Mheshimiwa Ndugai. *(Makofi)*

*Hapa (Mhe. Job Yustino Ndugai) Aliend a Mbele kwa ajili ya kuomba kura*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Tafadhali Mheshimiwa Ndugai karibu sana. Karibu sana Mheshimiwa Ndugai. *(Makofi)*

Mbele yako hapa kuna Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumekutana humu ndani leo na katika mkutano huu tukiwa na ajenda moja tu ya kufanya uchaguzi wa Spika, Kiongozi Mkuu wa Bunge letu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tunayo habari, tumetangaziwa kwamba wewe ndiyo mgombea pekee kwa Kiti hiki kwa sasa kutoka Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa utaratibu na heshima naomba nikupe nafasi ujieleze unayoona yanafaa kujieleza mbele ya Waheshimiwa Wabunge hawa na baadae nitawauliza Wabunge kama wana maswali ya kukuuliza. Karibu sana Mheshimiwa Ndugai. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa uliyonipa.

Waheshimiwa Wabunge Wateule, naitwa Job Yustino Ndugai, Mbunge Mteule wa Kongwa. Nianze kuwakaribisha wote mliotoka nje ya Dodoma, karibuni sana Dodoma na niwapongeze sana kwa kupita katika tanuri la Uchaguzi Mkuu salama na kuwa washindi. *(Makofi)*

Nimesimama mbele yenu kuwaomba kura ili nupate imani yenu ya kuwa Spika wa Bunge letu la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kuwa na afya njema na kuweza kukutana katika siku muhimu sana ya leo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani yake kwetu sote mpaka tumekuwa hapa, lakini pia nakishukuru chama chetu, Chama cha Mapinduzi kwa mchakato mzima ambao umetuwezesha wengi wetu tumekuwa hapa. *(Makofi)*

Hapa Bungeni minipa nafasi hii nitasimamia sana Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano, Kanuni zetu na taratibu mbalimbali. Ninachoweza kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge ni kwamba nitawatendea haki wote kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitalifanya Bunge hili la Kumi na Mbili liwe ni Bunge la mfano ambalo halijawahi kupatikana toka uhuru wa nchi yetu na mimi kama Mbunge mwenzenu

naelewa sana matatizo ya Waheshimiwa Wabunge, madhila ya Waheshimiwa Wabunge, wapi pana bana na katika mambo muhimu yale ndiyo nitakuwa mstari wa mbele kabisa, nafikiri tunaelewana. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa Waheshimiwa kutoka Kambi ya Upinzani najua mpo wachache tutawalinda sana kabisa mtaishi kwa raha bila tatizo lolote, hamtabaguliwa na mtafanya kazi yenu vizuri. Kwa Watanzania watarajie Bunge ambalo litawapa matokeo mazuri sana na mwisho wa siku watakubali kwamba Bunge la Kumi na Mbili limewatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kura za Wajumbe wote, lakini pia naomba kura yako Mwenyekiti. Ahsante sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Kwa heshima ya huyu anayejieleza sasa maana sasa hivi atageuka kuwa *boss* wangu, kwa hiyo na mimi nataka kusimama, nakushukuru sana kwa maelezo yako. Sasa Waheshimiwa Wabunge kama ilivyo ada tumezoea mikutano kama hii, kama kuna mtu anafikiri lazima aulize natoa nafasi.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ngojeni kwanza mimi ndiyo Mwenyekiti.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Hakuna.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida, Mbunge wa Nkasi.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na nina swali moja kwa mgombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgombea najua nafasi unayoiomba ni nafasi ambayo ulikuwa nayo kipindi kilichopita na wewe ni mwanadamu na mwanadamu yoyote ana mapungufu kama nilivyo mimi ninayekuuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemuomba mgombea atuambie Wabunge ambao tunategemea kumpa imani kwamba pamoja na nafasi uliyokuwa nayo bado kulikuwa na mapungufu kidogo kama binadamu ambayo ulifikiri na wewe uliyaona.

Je, katika Bunge hili unategemea kuonesha kipi cha tofauti kutokana na mapungufu machache ambayo yalitokea kipindi kilichopita? Ahsante.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Karibu.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na namshukuru sana Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kwa swali lake zuri.

Kwanza nianze kwa kumpongeza maana yake amemshinda rafiki yangu Ally Keissy na alikuwa akituambia hapa tutakutana JImboni na wamekutana kweli, kwa hiyo, hongera sana. *(Makofi/Kicheko)*

Nimhakikishie na nilisema katika maelezo yangu kwamba kwa kuwa Wabunge wa kutoka upande wa upinzani maana hatutakuwa na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa sababu hawataweza kutimiza asilimia 12.5 ambayo ipo katika Kanuni yetu, lakini niwahakikishie kabisa, uongozi kwa maana ya Spika na Wasaidizi wake wote Ofisi ya Bunge itawatendea haki kabisa, kabisa, kabisa lakini niwahakikishie Wabunge wa CCM ambao ni wengi hapa watawatendea haki kabisa na Bunge hili lina Wabunge vijana wengi sana na bahati nzuri Wabunge wa Upinzani walio wengi karibu wote isipokuwa wawili, watatu watakuwa ni akina mama, wasichana na Wabunge wengi vijana watawandea haki kabisa, wasiwe na wasi wasi kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Kuna swali? Basi kwa kuwa maswali yameisha nakuruhusu mgombea uende

ukakae, naam!! Wewe ni Mjumbe unakaa ndani, tafuta kiti ukae popote, naomba ukae umuunge mkono.

*Hapa (Mhe. Job Yustino Ndugai) Aliendа Kukaa*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Katibu kwa hatua zinazofuata.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge ambao wako ndani sasa hivi ni 263 na kwa hali hiyo tunaweza kuendelea na zoezi la uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba ipigwe kengele ili Wabunge wote wawemo ndani wakati tunafanya zoezi hili.

*(Hapa Kengele Ilipigwa)*

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:** Wahusika anza kugawa karatasi kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ajili sasa ya kupiga kura fanyeni hima.

Waheshimiwa Wabunge, naomba muangalie kwa makini, hayo makasha yamewekwa mbele ili muweze kuona kwamba sasa hayana kitu na kipindi hiki nina uhakika kabisa wote mtaona, hebu nyanyua juu ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuona. Nadhani mmeshuhudia?

Basi anzeni kugawa karatasi za kupiga kura.

*(Hapa Maafisa wa Bunge waligawa Karatasi za Kupigia Kura)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Wabunge mliopo nje muingie ndani. Labda kwa wageniu niwajulishe tu kwamba usipoingia humu ndani hata neema haikupati lazima geti lile lifunguke ndiyo neema utaisikia, kwa hiyo, waliopo nje naomba muingie.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:** Hakikisheni kila Mbunge anapata karatasi moja siyo mbili tafadhali, wale wanaogawa karatasi, karatasi moja kwa Mbunge

*(Hapa Maafisa wa Bunge waliendelea kugawa Karatasi za Kupigia Kura)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa wote mmepata karatasi?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Labda anyooshe mkono mtu ambaye hajapata karatasi, asiyepata!! Mheshimiwa Mbunge wa Mvumi subiri kidogo utatumbukiza tu. Wote tumepata karatasi? *(Kicheko)*

Katibu nafikiri vijana wako wakakusanye.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:** Kusanyeni, kusanyeni kura tayari.

*(Hapa Karatasi za Kura Zilikusanywa)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Tuharakishe kidogo, ratiba yetu leo si rafiki sana. Naomba wakati wote tunapofanya zoezi hili Waheshimiwa Wabunge tutulie kwenye viti vyetu.

Nadhani wote tumepiga kura, kama tumemaliza basi simameni hapo mbele na maboksi yenu kwanza, simameni hapo hapo, mmoja achukue kule huku bado huku, pale.

Nadhani wote tumekusanya, sasa nimuombe mgombea wa nafasi hii Mheshimiwa Ndugai tukuoe nafasi ututeulie mwakilishi wako, kama una mwakilishi au anamwamini msimamizi wa uchaguzi.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Naamini meza. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Haya, sasa katika hatua hii *Sergeant-At-Arms* njooni hapa na virungu vyenu msindikize hizi kura. Haya maboksi na wabebaji nendeni kwenye chumba cha kuhesabia kura, wasimame kidogo, Mheshimiwa Mbunge wa Mvumi.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na malalamiko ya mara kura zimeibiwa hatuwezi kuwa waangalizi ili kwenda kusimamia hilo zoezi kikamilifu?

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Kwa bahati mbaya mgombea anaamini meza. Kwa hiyo, mimi nimetuma askari tu hawa wenye kiapo wakalinde kwa bunduki huko ndani.

Sasa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tunataka zoezi hili lifanyike kwa ufasaha, tuhesabu halafu tuje kutoa matangazo hapa, tupumzike kidogo, natoa fursa tupumzike kidogo tutaanza kutoa matangazo saa 4:20 asubuhi. Kwa hiyo saa 4:15 asubuhi kila mmoja awe humu ndani.

Sasa naahirisha mpaka saa hiyo niliyoisema. Naomba tusiende mbali sana zoezi hili litachukua si zaidi ya nusu saa.

*(Saa 3:51 asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 4:15 Asubuhi)*

*(Saa 4:23 Asubuhi Bunge Lilirudia)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, haya tuingie ndani, nilikuwa naomba tuiingie ndani, waliopo *canteen* kule warudi, Mheshimiwa Mshua ukae kwenye kiti, kaa kwenye kiti Mheshimiwa Asha.

Waheshimiwa Wabunge, tunaomba tuingie ndani, matangazo yanayofuata ni muhimu sana. Ninyi vijana wa humu ndani mmoja aende *canteen* kule akawakumbushe Waheshimiwa Wabunge waingie ndani.

Tafadhali naomba tuingie ndani, najua Waheshimiwa wengi wana wageni huko nje, lakini watuvumilie kidogo, tuingie ndani tumalize hili zoezi. Tafadhali tuharakishe huko nje, nawaona pale kwenye *machine* mko wengi sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kazi ya kupiga kura, tumemaliza tayari kazi ya kuhesabu kura. Sasa naomba nimkaribishe Msimamizi wa Uchaguzi *(Returning Officer)*, Katibu wa Bunge ili aweze kutupa matokeo. Haya Katibu.

**MATOKEO YA UCHAGUZI WA SPIKA**

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaanza zoezi yaani kabla hatujapiga kura nilitangaza idadi ya Wajumbe waliokuwemo ndani walikuwa 263, lakini baadae idadi hiyo iliongezeka kufika 345 na wote 345 wamepiga kura. Kati ya kura zote 345, kura 344 zimesema ndiyo na kura iliyosema hapana ni moja. Kwa hiyo, kwa asilimia Mheshimiwa Job Yustino Ndugai amepata asilimia 99.7. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Ahsante sana Katibu kwa matangazo hayo.

Sasa nawaomba wafuatao waje hapa mbele niwatume, namuomba Mbunge wa Iringa Mjini Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kama yupo, hakuja? Loh. Mheshimiwa Najma, njoo mbele hapa, Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi Mheshimiwa Aida. Sasa kama Jesca hayupo basi aje Mheshimiwa Mbunge wa Lindi Mjini, yule wa Lindi Mjini yupo? Hayupo? Sogea hapa, hayupo, Mwenyekiti ndiye anayechagua.

Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum mzoefu wa Dar es Salam njoo na mimi nawatuma ninyi mkatuletee huyo Mheshimiwa Ndugai aingie humu ndani, mtafute kokote aliko, mtafuteni kokote aliko, mimi sijui aliko, lakini mtafuteni aje humu ndani.

Haya mtafuteni aingie humu ndani, mtafuteni Mheshimiwa Spika mteule aingie humu ndani ili aweze kula kiapo. Nimewaweka Wabunge wote wa zamani kwa sababu najua, mnajua kona zote za Bunge hili.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliotajwa walimtafuta na kumpata Mhe. Job Y. Ndugai na kumsindikiza eneo la kwenda kula Kiapo cha Uaminifu na Kiapo cha Spika)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Sasa kitendo kinachofuata ni Mheshimiwa Spika kuapa mbele ya Bunge hili. Baada ya hapo nitaeleza hatua nyingine inayofuata.*( Makofi/Vigelegele)*

## KIAPO CHA UAMINIFU NA KIAPO CHA SPIKA

1. Mhe. Job Yustino Ndugai

*Hapa (Mhe. Job Yustino Ndugai) Aliapa Kiapo cha Uaminifu na Kiapo cha Spika*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Katika hatua hii nakuomba Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano sasa ukavae joho lako ili uingie. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alitoka Nje ya Ukumbi na kwenda Kuvaa Joho la Spika*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Spika atakapokuwa anaingia tutasimama kwa heshima yetu tumkaribishe hapa ndani. Atakuja hapa mbele moja kwa moja kwenye kiti chake hapa, atatoa maneno ya shukrani na baada ya hapo ataanza kazi ya kutoa kiapo moja kwa moja, kwa hiyo akishamaliza kule ataingia.

Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kukamilisha zoezi hili muhimu la kihistoria. Tumeshampata Spika wetu ambaye amepita kwa kishindo kwa rekodi ambayo haijawahi kuwekwa. Tunae

sasa Spika Mheshimiwa Job Ndugai ndiye Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hiyo, viongozi wote wa mihimili wamekamilika. Tunaye Mheshimiwa Rais ambaye amepita kwa kishindo katika uchaguzi huu mkuu, Dokta John Pombe Magufuli, leo tumempata Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. Huyu sasa sio Spika Mteule ni Spika. *(Makofi)*

Nasi uteule utaisha, tutamuita humu ndani aje ili atuondoshee uteule na tuanze kuitwa Waheshimiwa Wabunge, maana yeye ameshaapa kiapo chake. Kwa hiyo, sasa naomba mumuingize ndani Mheshimiwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya hapo na cheo changu kitakuwa kimefutwa. *(Kicheko)*

*Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Aliingia Ukumbini na Kukalia Kiti*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa kazi inaanza. Wimbo wa Taifa, kwaya yetu ya Bunge.

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa na Kwaya ya Watumishi wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnaowaona waliotuimbia Wimbo wa Taifa ni watumishi wa Bunge letu la Tanzania tuwapigie makofi. Tunaendelea na Wimbo wa Afrika Mashariki kabla hatujaendelea. *(Makofi)*

**WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Uliimbwa na Kwaya ya Watumishi wa Bunge)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Mkiwa mmesimama hivyo hivyo, sasa ni wakati wa dua ya kuiombea nchi yetu na kuliombea Bunge.

## D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## SHUKRANI ZA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaweza kukaa.

Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa muda aliyetuongozea shughuli asubuhi ya leo, Mheshimiwa Lukuvi, kwa kuifanya kazi hiyo kwa weledi mkubwa na kuonesha uzoefu mkubwa alionao, tunakushukuru sana. Yeye ndiye Mbunge ambaye amekuwepo Bungeni mfululizo kwa muda mrefu kuliko Mbunge mwingine yeyote katika Bunge hili la 12. *(Makofi)*

Kwa Wabunge walioingia kwa mara ya kwanza hicho ndio kipimo, yeye hii ni mara ya sita anaingia Bungeni hapa. Kwa wewe uliyeingia mara ya kwanza sasa anza kuangalia kama *road map* hiyo inakufaa ili uweze kuwawakilisha watu wako kwa muda mrefu na kwa uhakika kama Mheshimiwa Lukuvi. Mtu mwingine aliyekaa muda mrefu mfululizo katika Bunge hili ni mimi mwenyewe, halafu anafuata Mheshimiwa Jenista na wengine. Tunawashukuru sana wananchi waliotuamini, si jambo dogo wala si rahisi hata kidogo. Mnaona hiyo mara moja tu mchakato wenyewe ulivyo ni shughuli pevu. *(Makofi)*

Nianze kwa kuwapa hongera sana wote kwa kuchaguliwa kwenu na kuaminiwa na wananchi wenu muweze kuwa wawakilishi wao katika nyumba hii ya Watanzania, karibuni sana. Ni heshima kubwa sana na matarajio ya Wananchi wetu ni makubwa sana kwa kila mmoja wetu. *(Makofi)*

Tunao wajibu mkubwa mbele yetu wa kuhakikisha kwamba hatuangushi matumaini ya Watanzania hawa waliotuamini tuwe wawakilishi wao katika nyumba hii Tukufu. Ninaamini kabisa kila mmoja hatasahau hata mara moja

jukumu la msingi la uwakilishi, kutunga sheria zilizo bora, kuhakikisha kwamba tunasimamia rasilimali za umma, tunaishauri Serikali yetu kwa kadri iwezekanavyo kwa ukweli na uwazi na tunamtendea haki kila Mtanzania.

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Rais wetu Dokta John Pombe Joseph Magufuli juzi wakati akiapishwa kuwa Rais wa Nchi hapa Dodoma alisema na kurudia mara tatu kwamba uchaguzi umekwisha, uchaguzi umekwisha, uchaguzi umeisha. Na kwa hiyo, kuanza kuapishwa kwa Waheshimiwa Wabunge hapa leo muda mfupi ujao ni kuendelea kupigia mstari ujumbe huo wa Mheshimiwa Rais kuwa uchaguzi umeisha. Kwa hiyo, sasa ni hapa kazi tu na Mungu atubariki sana katika kazi tunazoenda kuzifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu haitakuwa nyepesi, huo ndiyo ukweli, kazi yetu haitakuwa nyepesi, Bunge letu linapaswa kuwa la matokeo chanya kwa maendeleo ya Watanzania. Mipango ya nchi itapita hapa, bajeti ya nchi itapita hapa, sheria za nchi zitapita hapa, tutatunga mpya, tutarekebisha baadhi, tutafuta nyinginezo, chombo hiki ndicho Mshauri Mkuu wa Serikali, Bunge, kwa mambo yote. Serikali itakuja hapa kujibu maswali ambayo ninyi mtauliza kwa niaba ya wananchi. Uwajibikaji mkubwa wa Serikali unafanyika hapa, naamini kazi hiyo si kazi nyepesi, si kazi ndogo.

Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kabisa kwamba, Wabunge wengi wa Bunge la 12 wanatoka katika Chama cha Mapinduzi, lakini hilo halina maana kwamba Bunge hili sasa litakuwa la ndiyo, ndiyo! Wala haina maana kwamba Bunge hili litakuwa la hapana, hapana! ni Bunge ambalo mimi naamini litatekeleza wajibu wake kama ipasavyo na litakuwa ni la kutekeleza wajibu wake kweli kweli. Miongoni mwetu baadhi watateuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, na kadhalika, niwahakikishie hapa Bungeni watawajibika kweli kweli pamoja na wasaidizi wao, hakuna kubebana. *(Makofi)*

Niwape wosia, hasa Wabunge wageni na wengine waliokuwepo, ukichagua kuwa Mbunge bubu, usiyesema, unayejipendekeza, usidhani kwamba jambo hilo kwa wananchi wako lina tija. Ukichagua kuwa Mbunge bubu, husemi, upo upo tu, eti ili uonekane una nidhamu kwenye chama au mahali pengine umeliwa, huo ndio ukweli, utakuwa umejimaliza, ukidhani kunyamaza ndio nidhamu, siyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wananchi wamekuchagua kwa sababu wanaamini una uwezo wa kuwasemea na kusema mambo yao kuiambia Serikali, watafurahi sana wakiona mawazo yao na fikira zao zinawakilishwa vizuri hapa Bungeni. Na sisi tutajitahidi katika Bunge hili kuhakikisha kwamba taarifa nyingi za Bunge zinawafikia wananchi wetu kadri iwezekanavyo. Tunaomba Vyombo vya Habari vyote watoe kazi za Bunge ziwafikie wananchi haraka iwezekanavyo, tukijifungia hapa habari zisiwafikie wananchi Bunge hili litakuwa limehukumiwa toka mwanzo kwamba, kwa kuwa lina Wabunge wengi wa CCM ndiyo maana halisikiki, halifanyi kazi, halionekani.

Kwa hiyo, lazima Bunge hili lionekane, muonekane, msikike, mnavyoishauri Serikali na mnavyoiambia Serikali, na tuna hakika Serikali yetu siku zote ni sikivu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi itazichukua hoja zote na mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Kama nilivyosema mwanzo, ndugu zetu wa Upinzani ambao mko humu ndani, mna haki kabisa. Ninyi ni wachache *(minority),* lakini *minorities* wana haki zao. Wachache wana haki zao. Moja ya kazi kubwa za Kiti ni kuhakikisha kwamba na ninyi mnasikika, tena mnasikika kabisa, vizuri zaidi. Mlio wengi mkiwaachia wachache wasikike, kwenu! Lazima tusikike sote; wasikike, na sisi tusikike. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ya kusema ni mengi, lakini nimalizie kwa sababu tunataka kuanza kuapishana hapa muda siyo mrefu, naomba sana tusome Kanuni. Tuzipitie kwa umakini na kuzielewa. Humu ndani huwezi ku-*operate* bila

kuzijua Kanuni. Kwa hiyo, tuanze na Kanuni, tuzisome, tuzipitie, tuzirudie tena. Muda unavyokwenda tutazidi kuzi-*practise* na kuona zinavyofanya kazi.

Tumeandaa semina, mara baada ya Bunge hili kufungwa tutaanza taratibu za semina mbalimbali ambazo zitatusaidia sana katika kutufungua macho na kutusaidia kama Wabunge kujua nafasi yetu katika jamii; sisi ni viongozi, katika mfumo wa uongozi wa nchi, tuna-*fit* wapi?

Kule Jimboni, Mkoani, hapa katika nafasi za Kitaifa, tuna nafasi gani? Tunashirikiana na watu gani? *Role* yetu ni nini? Ipi ni *role* ya wenzetu, na kadhalika? Ni muhimu sana. Maana kuwa Mbunge siyo kila kitu, lazima kuna kazi nyingine za wenzetu tuzifahamu, mipaka yetu tuweze kuijua na kadhalika.

Pia tusome Kanuni kwa sababu humu Bungeni ziko taratibu mpaka za mavazi na kadhalika, tuzijue vizuri. Ukiiingia humu utatolewa nje kwa sababu hukuvaa sawa sawa. Waandishi wa habari watakukimbilia hapo, watakupiga picha, watazirusha, zitafika Jimboni. Basi wale wengine watashikilia hiyo hiyo! Mwaka 2025 ndiyo suala lenyewe, "alifukuzwa Bungeni, alikuwa amevaa ovyo ovyo!" Tuzijue vizuri hasa akina mama mavazi yetu yako *variable.*

Kwa hiyo huwa yanawachanganya wengine. Ni vizuri sana kujua aina ya mavazi ya kuvaa. Ni ukweli usiopingika ukija umevaa ovyo tutakutoa nje tu kwa sababu tunalinda Kanuni wala siyo kwa sababu nyingine yoyote. Mfano mdogo tu, unapokuwa na gauni lako, basi hakikisha kiwiko hiki kisiwe nje. Lazima gauni lako ukivaa liwe limeishia hapa. Hilo siyo vazi la Kibunge; au kama *car wash* hivi, ndiyo gauni hilo, hapana. Hilo ni huko nje na kadhalika.

Kwa hiyo, ni vitu vidogo vidogo lakini ni muhimu sana katika Bunge na kulinda heshima na hadhi ya Bunge. Wageni wetu pia wanaokuja kutembelea Bunge kuanzia sasa kwenda mbele, unapokuja Bungeni jipange, uvae vizuri, uje vizuri kwa sababu ni mahali ambapo pana heshima yake.

Basi, baada ya maneno haya tutaendelea kuambiana na kuelekezana yaliyo mengi kadri muda unavyokwenda. Vinginevyo, Bungeni ni mahali pazuri sana, ni mahali ambapo mta-*enjoy* na ndiyo maana hata ambao walikosa nafasi ya kurudi hapa wanapa-*miss* kweli kweli! Kwa sababu ni mahali pa mchanganyiko mkubwa sana. Mimi huwa napaita chuo kikuu hapa. Siyo rahisi kupata mchanganyiko wa aina hii katika nchi yetu katika taasisi yoyote ile. Siyo rahisi kabisa.

Hapa tuna watu wa kila aina, tuna *professions* mbalimbali, tuna watu wenye uzoefu mbalimbali. Hapa huwezi kukarikri; kuna watu wana elimu ile mnayoiita ninyi ndogo, au wengine wanaita ndogo, lakini wana akili kweli kweli. Hapa ndiyo unajifunza hasa kwamba katika nchi yetu mambo yakoje. *(Makofi)*

Kwa hiyo, karibuni sana. Kama kiongozi nawahakikishieni haki zenu, mambo yenu yote tutayalinda kwa kadri iwezekanavyo na kama kuna jambo usisite kumwona Spika. Tukikaa hapa usisite kuniandikia ki-*note* na kuniambia kuna hili haliendi sawa, hasa kuhusu mambo yetu ya utaratibu yale, kama utaratibu haujakaa sawa sawa, basi tuuweke sawa sawa.

Mwisho kabisa, asije akakusogelea mtu kusema umkopeshe. Kweli kabisa! sikupaswa niliseme hivi, lakini mniwie radhi niseme. Tulipata taabu sana kwenye Bunge lililopita. Kwa hiyo, mkikopeshana huko, mimi simo jamani toka asubuhi. Atakuja mtu na lugha nzuri sana, siyo kweli, unaingia mkenge. *(Makofi/Kicheko)*

Basi baada ya maneno hayo, Katibu sasa tuendelee.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Kiapo cha Uaminifu kwa Wabunge.

**SPIKA:** Tunaanza utaratibu wa Kiapo cha Uaminifu. Tunaendelea. Leo tutakwenda kwa kadri tuwezavyo na pia kesho kadri tuwezavyo. Endapo kwa leo una udhuru fulani,

basi kama umo katika orodha ya leo, jitahidi ulete ujumbe mapema kwangu au kwa Katibu wa Bunge ili tukupangie kesho.

Wale wenye wageni pia mwapange vizuri ili kwa yule ambaye ameshaapishwa, basi atoke nje na wageni wake waweze kupiga picha za kumbukumbu na kuwaruhusu wale ambao wanaendelea kuapishwa ili wageni wao waweze kushuhudia zoezi linavyoendelea.

Ninawashukuru sana. Sasa tuendelee.

**KIAPO CHA UAMINIFU KWA WABUNGE**

2. Mhe. Prof. Adelardus Lubango Kilangi
3. Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa
4. Mhe. Dkt. Tulia Ackson
5. Mhe. William Vangimembe Lukuvi
6. Mhe. Mussa Azzan Zungu
7. Mhe. Najma Murtaza Giga
8. Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi
9. Mhe. Tarimba Gulam Abbas
10. Mhe. Rashid Abdalla Rashid
11. Mhe. Abdallah Dadi Chikota
12. Mhe. Abdallah Hamis Ulega
13. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo
14. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood
15. Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi
16. Mhe. Abeid Ramadhan Ighondo
17. Mhe. Aboubakar Damian Assenga
18. Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda
19. Mhe. Agness Elias Hokororo
20. Mhe. Agness Mathew Marwa
21. Mhe. Katani Ahmadi Katani
22. Mhe. Ahmed Ally Salum
23. Mhe. Ahmed Juma Ngwali
24. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby
25. Mhe. Aida Joseph Khenani *(Makofi/Vigelegele)*
26. Mhe. Salim Alaudin Hasham
27. Mhe. Aleksia Asia Kamguna

28. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti
29. Mhe. Ally Hassan Omar King
30. Mhe. Ally Khamis Yahaya
31. Mhe. Ali Vuai Khamis
32. Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa
33. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage
34. Mhe. Munde Tambwe Abdallah
35. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete
36. Mhe. Ally Anyigulile Mlagila Jumbe
37. Mhe. Ali Juma Makoa
38. Mhe. Ally Mohamed Kassinge
39. Mhe. Twaha Ally Mpembenwe
40. Mhe. Yahya Ali Mhata
41. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi
42. Mhe. Aloyce John Kamamba
43. Mhe. Amina Ali Mzee
44. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga
45. Mhe. Amina Bakar Yussuf
46. Mhe. Amina Daudi Hassan
47. Mhe. Amina Idd Mabrouk
48. Mhe. Haji Amour Haji
49. Mhe. Anastazia James Wambura *(Makofi/Vigelegele)*
50. Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi
51. Mhe. Eng. Andrea Mathew Kundo
52. Mhe. Angelina Adam Malembeka
53. Mhe. Dkt. Angelina Sylivester Lubala Mabula
54. Mhe. Anna Richard Lupembe
55. Mhe. Anthony Peter Mavunde
56. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi
57. Mhe. Anton Albert Mwantona
58. Mhe. Asha Abdullah Juma
59. Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji
60. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga
61. Mhe. Assa Nelson Makanika
62. Mhe. Asya Sharifu Omar
63. Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye
64. Mhe. Athuman Almas Maige
65. Mhe. Vuma Augustine Holle
66. Mhe. Bahati Keneth Ndingo
67. Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu

68. Mhe. Boniface Mwita Getere
69. Mhe. Boniventura Destery Kiswaga
70. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli
71. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa
72. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata
73. Mhe. Boniface Nyangindu Butondo
74. Mhe. Catherine Valentine Magige
75. Mhe. Cecil David Mwambe
76. Mhe. Charles John Mwijage
77. Mhe. Charles Muguta Kajege
78. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei
79. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava
80. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma
81. Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka
82. Mhe. Benaya Liuka Kapinga
83. Mhe. Constantine John Kanyasu
84. Mhe. Daimu Iddi Mpakate
85. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro
86. Mhe. Daniel Awack Tlemai
87. Mhe. Venant Daudi Protas
88. Mhe. Njalu Daudi Silanga
89. Mhe. Fredrick Edward Lowassa
90. Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe
91. Mhe. David Ernest Silinde
92. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile
93. Mhe. Dennis Lazaro Londo
94. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika
95. Mhe. Deogratius John Ndejembi
96. Mhe. Deus Clement Sangu
97. Mhe. Dorothy George Kilave
98. Mhe. Doto Mashaka Biteko
99. Mhe. Dunstan Luka Kitandula
100. Mhe. Esther Lukago Midimu
101. Mhe. Edward Kisau Olelekaita
102. Mhe. Edwin Enosy Swalle
103. Mhe. Elias John Kwandikwa
104. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu
105. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe
106. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi
107. Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni

108. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka
109. Mhe. Ester Edwin Maleko
110. Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe
111. Mhe. Fakharia Shomari Khamis
112. Mhe. Fatma Hassan Toufiq
113. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile
114. Mhe. Dkt. Festo John Dugange
115. Mhe. Flatei Gregory Massay
116. Mhe. Florent Laurent Kyombo
117. Mhe. Francis Kumba Ndulane
118. Mhe. Francis Leonard Mtega
119. Mhe. Furaha Ntengo Matondo
120. Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe
121. Mhe. Geofrey Mizengo Pinda
122. Mhe. Kapt. George Huruma Mkuchika
123. Mhe. George Natany Malima
124. Mhe. George Runwell Mwenisongole
125. Mhe. Ghati Zephania Chomete
126. Mhe. Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe
127. Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel
128. Mhe. Eng. Hamad Masauni Yussuf
129. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah
130. Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma
131. Mhe. Hamis Hussein Mwagao Tabasam
132. Mhe. Hamis Shabani Taletale
133. Mhe. Khamis Hamza Khamis Chilo
134. Mhe. Hassan Selemani Mtenga
135. Mhe. Hamad Hassan Chande
136. Mhe. Kassim Hassan Haji
137. Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla
138. Mhe. Simai Hassan Sadiki
139. Mhe. Hassan Zidadu Kungu
140. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma
141. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma
142. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako
143. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi
144. Mhe. Nicodemas Henry Maganga
145. Mhe. Abdi Hija Mkasha
146. Mhe. Husna Juma Sekiboko
147. Mhe. Hadija Shabani Taya

148. Mhe. Hussein Mohamed Bashe
149. Mhe. Ravia Idarus Faina
150. Mhe. Dkt. David Mathayo David
151. Mhe. Nicholaus George Ngassa
152. Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma
153. Mhe. Innocent Edward Karogeris
154. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa
155. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate
156. Mhe. Irene Alex Ndyamkana
157. Mhe. Joseph Michael Mkundi
158. Mhe. Francis Isack Mtinga
159. Mhe. Issa Ali Mchungahela
160. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu
161. Mhe. Omar Issa Kombo
162. Mhe. Jackline Kainja Andrea
163. Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa ushirikiano ambao tumepeana asubuhi ya leo, kazi yetu inaendelea vizuri tena kwa *speed* nzuri sana. Kwa hiyo tutaendelea jioni ya leo kuanzia saa 11.00 jioni, naomba tuwahi, hata tuliokwishaapa basi tuje ili tuwaunge mkono wenzetu katika zoezi hili linaloendelea.

Kuna Mheshimiwa amepoteza mkebe wenye vitambulisho vyake, vikiwemo kalamu na kadi za benki na vitambulisho vingine, anaomba kama umechukua hasa eneo letu lile la kukaguliwa, basi uweze kuleta kwa Makatibu Mezani ili warekebishe. Pia Mheshimiwa mwingine amechukua miwani isiyo ya kwake ameacha ya kwake, basi akileta hapa mezani itaipata iliyo ya kwake.

Kwa kuwa tutaendelea jioni, basi kama kuna matangazo mengine tutaendelea kupeana, nawaomba tuwahi hiyo Saa 11.00 ili tuweze kuwa pamoja. Baada ya hayo, naomba kuchukua fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi leo jioni saa kumi na moja kamili.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Kiapo cha Uaminifu kwa Wabunge.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda siyo mrefu tutaendelea na shughuli ya kiapo. Shughuli yetu kama nilivyosema asubuhi inaenda vizuri sana. Tunaomba tu zile hati tunazowapatia baada ya kuwa mmeshafanya shughuli ya kiapo, ikiwezekana mturudishie leo. Mliozisahau, basi mturudishie kesho asubuhi mapema kwa sababu ni muhimu sana kwa ajili ya mambo yanayohusu utaratibu, hasa inapofika mwisho wa mwezi huu. Ukichelewesha, basi utakuwa humo kwenye utaratibu, mpaka labda mwezi ujao wakati wa *Christmass* na nini. Kwa hiyo, nafikiri mmenisoma.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kunielewa. *(Makofi)*

Ahsante, tunaendelea na kiapo sasa.

164. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa
165. Mhe. Wanu Hafidh Ameir *(Makofi)*
166. Mhe. Jackson Gideon Kiswaga
167. Mhe. Subira Kbhamis Mgalu
168. Mhe. Priscus Jacob Tarimo
169. Mhe. Festo Richard Sanga
170. Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa
171. Mhe. Margaret Simwanza Sitta
172. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara
173. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo
174. Mhe. Condester Mundi Michael Sichalwe
175. Mhe. Shabani Omari Shekilindi
176. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi
177. Mhe. Jafari Wambura Chege
178. Mhe. Alfred James Kimea

179. Mhe. Janejelly James Ntate
180. Mhe. Janeth Elias Mahawanga
181. Mhe. Janeth Maurice Masaburi
182. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga
183. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza
184. Mhe. Jenista Joachim Mhagama
185. Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi
186. Mhe. Jerry William Silaa
187. Mhe. Jesca Jonathan Msambatavangu
188. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa
189. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo
190. Mhe. John Marko Sallu
191. Mhe. Jonas Van Zeeland
192. Mhe. Jonas William Mbunda
193. Mhe. Joseph Anania Tadayo
194. Mhe. Joseph George Kakunda
195. Mhe. Joseph Kizito Mhagama
196. Mhe. Joseph Zacharious Kamonga *(Makofi/Vigelegele)*
197. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege
198. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke
199. Mhe. Josephine Tabitha Chagula
200. Mhe. Judith Salvia Kapinga
201. Mhe. Juliana Daniel Shonza
202. Mhe. Juliana Didas Masaburi *(Makofi/Vigelegele)*
203. Mhe. Juma Hamad Omar
204. Mhe. Mbarouk Juma Khatib
205. Mhe. Ali Juma Mohamed
206. Mhe. Jumaa Hamidu Aweso
207. Mhe. Jumanne Abdallah Sagini
208. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba
209. Mhe. Kabula Enock Shitobelo
210. Mhe. Khamis Kassim Ali
211. Mhe. Iddi Kassim Iddi
212. Mhe. Kenneth Ernest Nollo
213. Mhe. Khadija Hassan Aboud
214. Mhe. Khalfan Aeshi Hilary
215. Mhe. Amour Khamis Mbarouk
216. Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo
217. Mhe. Latifa Khamis Juakali
218. Mhe. Justin Lazaro Nyamoga

219. Mhe. Leah Jeremiah Komanya
220. Mhe. Noah Lemburis Saputu Mollel
221. Mhe. Lucy John Sabu
222. Mhe. Maimuna Salum Mtanda
223. Mhe. Haji Makame Mlenge
224. Mhe. Mariamu Madalu Nyoka
225. Mhe. Martha Festo Mariki
226. Mhe. Martha Jachi Umbulla
227. Mhe. Mary Francis Masanja
228. Mhe. Maryam Azan Mwinyi
229. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan
230. Mhe. Maryam Omar Said
231. Mhe. Maryprisca Winfred Mahundi
232. Mhe. Masache Njelu Kasaka
233. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki
234. Mhe. Mohammed Maulid Ali
235. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani
236. Mhe. Michael Costantino Mwakamo
237. Mhe. Minza Simon Mjika
238. Mhe. Mohamed Lujuo Monni
239. Mhe. Soud Mohammed Jumah
240. Mhe. Moshi Selemani Kakoso
241. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo
242. Mhe. Muharamy Shabani Nkenge
243. Mhe. Mussa Hassan Mussa
244. Mhe. Salim Mussa Omar
245. Mhe. Munira Mustafa Khatib
246. Mhe. Mussa Ramadhani Sima
247. Mhe. Mwanaidi Ali Khamisi
248. Mhe. Eng. Mwanaisha Ulenge
249. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said
250. Mhe. Maida Hamad Abdallah
251. Mhe. Mwantakaje Haji Juma
252. Mhe. Mwantumu Dau Haji
253. Mhe. Mwantumu Mzamili Zodo
254. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu
255. Mhe. Mustafa Mwinyikondo Rajab
256. Mhe. Michael Mwita Kembaki
257. Mhe. Nancy Hassan Nyalusi
258. Mhe. Nashon William Bidyanguze

259. Mhe. Hussein Nassor Amar
260. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro
261. Mhe. Neema Gerald Mwandabila
262. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani
263. Mhe. Nora Waziri Mzeru
264. Mhe. Omari Mohamed Kigua
265. Mhe. Oran Manase Njeza
266. Mhe. Juma Othman Hija
267. Mhe. Patrick Alois Ndakidemi
268. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato
269. Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango
270. Mhe. Philipo Augustino Mulugo
271. Mhe. Dkt. Pindi Hazara Chana
272. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya
273. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan
274. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo
275. Mhe. Ridhiwan Jakaya Mrisho Kikwete
276. Mhe. Robert Chacha Maboto
277. Mhe. Rose Vicent Busiga
278. Mhe. Saada Mansour Hussein
279. Mhe. Maulid Saleh Ali
280. Mhe. Khalifa Salum Suleiman
281. Mhe. Santieli Erick Kirumba
282. Mhe. Jafar Sanya Jusa
283. Mhe. Sebastian Simon Kapufi
284. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali
285. Mhe. Seif Salum Seif
286. Mhe. Pascal Patrobas Katambi
287. Mhe. Selemani Jumanne Zedi
288. Mhe. Shaiff Mansour Jamal
289. Mhe. Sillo Daniel Baran
290. Mhe. Sylvestry Francis Koka
291. Mhe. Simon Songe Lusengekile
292. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo
293. Mhe. Selemani Said Jafo
294. Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato
295. Mhe. Mohamed Suleiman Omar
296. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo
297. Mhe. Dkt. Thea Merdad Ntara
298. Mhe. Timotheo Paul Mnzava

299. Mhe. Juma Usonge Hamad
300. Mhe. Ussi Salum Pondeza
301. Mhe. Vicent Paul Mbogo
302. Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil
303. Mhe. Zubeida Khamis Shaib
304. Mhe. Zulfa Mmaka Omar

*(Waheshimiwa Wabunge waliotajwa hapo juu waliapa Kiapo cha Uaminifu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunarejea tena. Tunashukuru sana kwamba leo tumeweza kwenda hatua kubwa, kazi yetu ya kuapisha itakamilika kesho, labda atayebaki ni mtu ambaye ana udhuru ambayo tunaweza tukaifanya siku inayofuata alfajiri, lakini Wabunge karibu wote tutamaliza kufanya shughuli ya kiapo kesho.

Niendelee kuwakumbusha tena karatasi zile za njano tuzirudishe. Ni vizuri ukaisaini tu hapa hapa na ukawapa Watumishi wetu wa Bunge wenye *uniform* za *blue* wakaweza kuzileta hapa mezani ili mambo mengine ya utaratibu yaweze kuendelea kwa haraka sana. *Immediately* tukimaliza kuapisha basi tuwe nazo zote kwa sababu watakaochelewa watakuwa wamechelewa *train* ya *SGR*. *(Kicheko)*

Baada ta maneno hayo najua leo Waheshimiwa Wabunge mna wageni wengi sana kutoka sehemu mbalimbali, majimboni, marafiki, ndugu na jamaa, kwa hiyo ni vizuri kutoka mapema kidogo ili kwenda kuangalia mambo yanayoendana na utaratibu, natambua hilo sana.

Tunawaomba sana Waheshimiwa Wabunge Mji huu wa Dodoma ni salama sana, lakini siku zote kuchukua tahadhari ni muhimu sana. Ni vizuri kutozagaa maeneo ambayo unaweza ukapata matatizo kidogo pembezoni huko kusikoeleweka. Ukipata shida hata wapiga kura watakuwa wanajiuliza hivi alifuata nini huko kwenye vichochoro? Kwa hiyo, hadhi yenu inawataka kwanza kurudi nyumbani mapema, lakini kuwa katika maeneo ambayo yanastahili Mheshimiwa uwepo, kwa hiyo nawatakia jioni njema.

Sasa nichukue nafasi hii kusitisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.46 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 11 Novemba, 2020 Saa 3.00 Asubuhi)*